

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

*Dar es Salaam
08 Mei, 2024*

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**RAIS SAMIA AZINDUA MKAKATI WA TAIFA WA MATUMIZI YA NISHATI
SAFI YA KUPIKIA**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa sekta binafsi nchini kuongeza uwekezaji na upatikanaji wa nishati safi ya kupikia katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, Rais Samia amewataka kuleta teknolojia rahisi itakayowezesha wananchi kupata nishati safi kadri ya uwezo wao pamoja na kulipia kulingana na matumizi kama inavyofanyika katika umeme.

Rais Samia ametoa wito huo leo katika hafla ya uzinduzi wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 -2034 iliyofanyika katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC).

Rais Samia pia amesema Mkakati huo unatoa mwongozo wa kitaifa kwa wadau wote kuhakikisha nchi inafikia lengo ililojiwekea la 80% ya Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Vile vile, Rais Samia amesema lengo la Mkakati huo likitekelezwa na kutimia litapunguza gharama ya nishati safi ya kupikia pamoja na kuongeza upatikanaji na uwekezaji wa nishati safi.

Rais Samia amebainisha kuwa Mkakati huo wa kitaifa pia utachangia jitihada za Serikali za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kutokana na uharibifu wa misitu ambao huchangiwa na shughuli za kibinadamu.

Kwa sasa, inakadiriwa kuwa takribani hekta 469,000 za misitu hupotea kila mwaka ambapo nishati za kuni na mkaa ni moja ya chanzo kikuu cha kutoweka kwa misitu hiyo.

A handwritten signature in blue ink.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu